Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# JARIDA
## la Mtandaoni la NSSF

### Matukio yaliyotikisa kuanzia Januari – Disemba, 2023




Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

**NSSF**


Simu Bure
0800116773

@NssfTanzania

# MALI ZA KAMPUNI ZAPIGWA MNADA KULIPA MICHANGO YA WANACHAMA WA NSSF

**Na MWANDISHI WETU**

Mali za kampuni ya uzalishaji wa majani ya chai ya Rift Valley Tea Solution Limited, ambazo ni mitambo ya uzalishaji majani ya chai zimepigwa mnada na kampuni ya udalali wa Mahakama FreedomPath Tanzania Limited, kwa idhini ya Mahakama ya Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam, katika shauri la madai namba 93/2022.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Januari 23, 2023, Mkurugenzi Mtendaji wa FreedomPath Tanzania Limited, Bw. Deusdedit Kabunduguru, amesema katika shauri hilo mdai ni Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), dhidi ya kampuni hiyo ambayo ilishindwa kuwasilisha fedha za michango ya wafanyakazi wake NSSF, ambapo Mfuko uliamua kufungua kesi Mahakamani ili mwajiri huyo aweze kulipa michango ya wafanyakazi wake ambayo ipo kwa mujibu wa sheria.

Naye, Bw. Geofrey Sikira ambaye ni Kaimu Meneja Mwendesha Mashauri wa NSSF, amesema Mfuko kwa amri ya Mahakama imeuza mali ya mwajiri huyo baada ya kushindwa kulipa michango ya wanachama wake kwa mujibu wa sheria. "Mwajiri anapaswa kuwasilisha michango ya wanachama wake kila mwezi na akikaa kwa miezi sita bila kuwasilisha anakuwa ni mdaiwa na hivyo anachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kufikishwa Mahakamani," amesema Bw. Sikira.



# NSSF YATEKELEZA KWA VITENDO MAELEKEZO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

**Na MWANDISHI WETU**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), umetekeleza kwa vitendo maagizo yaliyotolewa na Serikali ya Awamu ya Sita ya kupunguza gharama ili kuwaondolea kero wananchi na watumiaji wa Daraja la Nyerere, Kigamboni, Dar es Salaam.

Hatua hiyo imekuja baada ya Mfuko kuzindua rasmi mfumo wa 'NSSF Bridge Portal' ambao unawezesha mteja kununua bando la siku, wiki au mwezi ili kupita na chombo cha moto katika Daraja la Nyerere.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa mfumo huo tarehe 21 Februari, 2023, Mkurugenzi wa TEHAMA wa NSSF, Bw. Donald Mhaiki, amesema Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na NSSF ulipitia gharama za tozo za Darajani kwa vyombo vya moto vinavyopita katika daraja hilo na kufanya punguzo kubwa la tozo.

Bw. Mhaiki amesema punguzo hilo lilianza kutumika rasmi mwezi Mei, mwaka 2022, ambapo Mfuko ulikuja na punguzo zaidi kwa kuanzisha mfumo wa bando ambapo mtumiaji wa Daraja anaweza kupita kwa kulipia kwa siku, wiki au mwezi.

Kabla ya kuanza kwa mfumo huo, mtumiaji wa Daraja alikuwa anatumia wastani wa shilingi 90,000 kwa mwezi, lakini kwa kutumia mfumo huu mtumiaji anatumia shilingi 35,000 kwa mwezi.

Naye, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Bi. Lulu Mengele, amesema NSSF inaishukuru Serikali ya awamu ya sita iliyotoa maelekezo ya kupunguza gharama ili kuondoa kero kwa wananchi na watumiaji wa Daraja la Nyerere.

Baadhi ya wakazi wa Kigamboni akiwemo Bi. Naomi Charles amesema wanaipongeza Serikali kupitia NSSF kwa kuja na huduma ya bando ambayo ni nzuri kwani inapunguza gharama kubwa ya kuvuka Darajani.



# NSSF YATOA MSAADA WA VIFAA TIBA MKOANI MOROGORO

**Na MWANDISHI WETU**

Katika kuelekea siku ya wanawake duniani, wafanyakazi wanawake wa NSSF, walitoa msaada wa vifaa tiba katika kituo cha afya cha Chazi kilichopo wilayani Mvomero Mkaoni Morogoro, ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya NSSF ya Uchangiaji na Udhamini (CSR) katika jamii.

Vifaa tiba hivyo vilikabidhiwa tarehe 2 Februari, 2023 na baadhi ya wafanyakazi wanawake wa NSSF wakiongozwa na Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma, Bi. Lulu Mengele ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu, Masha Mshomba. Miongoni mwa vifaa tiba vilivyokabidhiwa katika kituo hicho ni pamoja na jokofu la kuhifadhia damu kwa lengo la kuokoa maisha ya wananchi wakiwemo wajawazito wanaoenda kujifungua katika kituo hicho.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Dkt. Philipina Philipo aliishukuru NSSF kwa msaada huo ambao utasaidia kuokoa Maisha ya wananchi wa eneo hilo.




# 'HONGERENI NSSF NI KITU KIZURI'

**Na MWANDISHI WETU**

Kauli hiyo ilitolewa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati alipotembelea mradi wa ujenzi wa hoteli ya kitalii ya nyota tano inayomilikiwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi wa Jamii (NSSF).

"Hongereni sana kwa kweli ni kitu kizuri na kabla ya maelezo nilikuwa nina mashaka mashaka nikasema sasa hiki kitu huku Mwanza kitarudisha kweli 'economic value' ya hiki kitu iko wapi na 'retune of investment' iko wapi," amesema.

Mhe. Rais Dkt. Samia alifanya ziara ya kutembelea mradi huo uliopo eneo la Capripoint jijini Mwanza tarehe 14 Juni, 2023, ambapo baada ya kupata maelezo ya mradi huo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba na kwa Meneja Miradi wa NSSF, Mhandisi Helmes Pantaleo, alisema hana mashaka kuhusu mradi huo kwani wataalamu watakuwa wameshapiga mahesabu.

Amesema vitega uchumi vya aina hiyo vitaongeza tija kwenye Mfuko huku akiwasisitiza wafanyakazi kuendelea kutoa huduma bora na kuacha tamaa wanapotekeleza majukumu yao.

Kwa upande wake, Mhe. Patrobas Katambi amesema miradi ya aina hiyo ili ipitishwe ni lazima Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ishauri na Ofisi ya Waziri Mkuu inasimamia na kuwa lengo kubwa la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza ni kulinda fedha za Mifuko.

Akizungumzia maelezo kuhusu mradi huo, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Bw. Masha Mshomba amesema ujenzi wa hoteli hiyo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2024, na kuwa utachangia shughuli za uchumi za jiji la Mwanza.



# JAJI KIONGOZI AFUNGUKA

## Awataka Majaji na Mahakimu kuyapa kipaumbele mashauri yanayohusu hifadhi ya jamii

**Na MWANDISHI WETU**

Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Mustapher Siyani amewataka Waheshimiwa Majaji na Mahakimu nchini, kuyapa kipaumbele mashauri yote yanayohusu sekta ya hifadhi za kijamii.

Mhe. Jaji Siyani amesema hayo tarehe Juni 9, 2023 wakati akifungua semina ya siku mbili kwa njia ya mikutano mtandao (e-Mikutano) kwa Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wa Kanda ya Ziwa, Tabora, Manyara na Kigoma iliyofanyika jijini Mwanza.

Amesema kupitia semina hiyo, NSSF imefungua njia ambayo wadau wengi wataifuata, hivyo Mahakama na NSSF kama ilivyo kwa taasisi nyingine zinazotoa huduma kwa jamii haziwezi kufanikiwa ikiwa kila taasisi itajifungia ikiamini inaweza. "Niwahakikishie wadau wetu wote wakiwemo NSSF kuwa Mahakama ya Tanzania itaendelea kuwashirikisha katika mipango yake na hususan inapotekeleza mpango mkakati wake wa miaka mitano utakaokamilika ifikapo mwaka 2025," alisema.

Naye, Rais wa Chama Cha Majaji na Mahakimu Tanzania (JMAT),

Mhe. Jaji John Kahyoza aliushukuru uongozi wa NSSF kwa kuwawezesha kupata mafunzo hayo ambayo ni moja ya utekelezaji wa malengo makuu ya chama hicho ambacho lengo lake ni kulinda uhuru wa Mahakama na kujenga ujuzi kwa Majaji na Mahakimu Tanzania.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani, Bw. Godfrey Ngonyani, amesema ushirikiano baina ya Mfuko na muhimili huo ni muhimu na ni sehemu ya mkakati wa NSSF kuendelea kushirikiana na wadau, ikiwemo kuandaa vikao na semina.






# HABARI PICHA

## USHIRIKI WA NSSF MAONESHO YA SABASABA 2023











## USHIRIKI WA NSSF MAONESHO YA NANENANE 2023










# NSSF YAWAFIKIA WACHIMBAJI, YATOA ELIMU NA KUTATUA KERO ZA WANACHAMA

**Na MWANDISHI WETU**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulishiriki na kutoa huduma zake zote katika Maonesho ya Sita ya Kimataifa ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika Mkoani Geita, yaliyobeba kauli mbiu isemayo 'Matumizi ya Teknolojia Sahihi katika Kuinua Wachimbaji Wadogo Kiuchumi na Kuhifadhi Mazingira'

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Bw. Masha Mshomba, amesema kupitia maonesho hayo NSSF ilitoa elimu pamoja na kuongeza uelewa wa hifadhi ya jamii kwa makundi mbalimbali kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi kama vile wachimbaji wadogo wa madini, wakulima, wafugaji, wavuvi, mamalishe, bodaboda na wajasiriamali wengine wote ili waweze kujiunga na kujiwekea akiba kwa maisha yao ya sasa na ya baadaye.

Amesema maonesho hayo yalikuwa muhimu kwa Mfuko kwa kuwafikia wananchi waliojiajiri wenyewe na kuwapatia elimu ya hifadhi ya jamii ili waweze kujiunga na kujiandikisha kwa ajili ya kujiwekea akiba, huku NSSF ikitatua kero mbalimbali kwa wanachama na wadau.



# MATUKIO KATIKA PICHA ZIARA YA MWENYEKITI WA BODI YA NSSF MAKAO MAKUU









# HABARI PICHA

## USHIRIKI WA NSSFWIKI YA HUDUMA KWA WATEJA 2023










## USHIRIKI WA NSSF WIKI YA VIJANA 2023












# HABARI PICHA

## BODI YA WADHAMINI YA NSSF YATEMBELEA MRADI WA KIWANDA CHA SUKARI MKULAZI












# DIRA NA DHIMA NSSF

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

## DIRA

Kuwa mtoa huduma wa kuaminika na endelevu katika sekta ya Hifadhi ya Jamii

## DHIMA

Kutoa huduma bora za hifadhi ya jamii kwa wanachama, kupitia watumishi wenye weledi, ubunifu na ari ya kazi kwa kutumia teknolojia sahihi

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF),
Jengo la Benjamin William Mkapa, Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 1322, Dar es Salaam, Tanzania

**Simu Bure: 0800116773,**
**Barua pepe: customercare@nssf.go.tz**
**Tovuti: www.nssf.go.tz**

**@NssfTanzania**